
يقين
YAQEEN
مكتب الدعوة والإرشاد بالمعذر وأم الحمام



باللغة السواحيلية

# فضل الإسلام

# ADHILA/UBORA WA UISLAMU


HEIKH MUHAMMAD IBN ABDULWAHAAB (ALLAH AMREHEMU)
FASIRI SHEIKH: HAMZA RAJABU SEFU
MEPITIWA NA SHEIKH: YASSINI TWAHA

للشيخ: محمد بن عبد الوهاب -رحمه الله-
مترجم: الشيخ حمزة رجب سيف
محقق: الشيخ ياسين طه

# فضل الإسلام

# FADHILA/UBORA WA UISLAMU

للشيخ: محمد بن عبد الوهاب رحمه الله

مترجم: الشيخ حمزة رجب سيف

محقق: الشيخ ياسين طه


SHEIKH MUHAMMAD IBNI ABDILWAHAAB (ALLAH AMREHEMU)

MFASIRI SHEIKH: HAMZA RAJABU SEFUKIMEPITIWA NA SHEIKH: YASSINI TWAHA

بسم الله الرحمن الرحيم

# MLANGO UNAOELEZEA UBORA WA UISLAMU

**Ni kauli yake Allah:** (Leo nimekukamilishieni dini yenu, na nimekutimizieni neema yangu, na nimekuridhieni/kupendeleeni UISLAMU kuwa ndio dini yenu).(Al-Maaida: 3).

**Na kauli ya Allah:** (Sema: Enyi watu! Ikiwa mnashaka katika Dini yangu, basi Mimi siwaabudu mnaowaabudu nyinyi badala ya Mwenyezi Mungu. Lakini Mimi namuabudu Mwenyezi Mungu anaye kufisheni. Na nimeamrishwa niwe miongoni mwa Waumini). (Yunus: 104).

**Na kauli yake Allah:**(Enyi mlioamini! Mcheni Mwenyezi Mungu, na Muaminini Mtume Wake, Atakupeni sehemu mbili katika rehema Zake, na Atakujaalieni muwe na nuru ya kwenda nayo. Na Atakusameheni.Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye kusamehe Mwenye kurehemu). (Al-Hadiid: 28).

*Na hadithi iliyo katika sahihi kutoka kwa Mtoto wa Omar (r.a) kwamba Mtume (s.a.w) Alisema: Mfano wenu na mfano wa watu waliopewa Kitabu (Mayahudi na Manaswaara) ni kama mfano wa Mtu aliyempa mtu ajira akasema: Ni nani atakayenifanyia kazi toka asubuhi mpaka nusu/katikati ya mchana kwa malipo ya Qiratwi moja? (Qiratwi ni aina ya malipo ambayo kwasasa yanatofautiana katika mizani na kiasi), Mayahudi

wakafanya(wakalipwa), kisha Akasema tena: Ni nani atakayenifanyia kazi toka nusu ya mchana mpaka muda wa Sala ya Alasiri kwa malipo ya Qiratwi moja? Manaswara wakafanya, (wakalipwa), kisha Akasema tena: Ni nani atakayenifanyia kazi toka swala ya Alasiri mpaka litakapozama jua kwa malipo ya Qiratwi mbili? Basi hao ni nyie (Waisilamu), Mayahudi na Manaswara wakakasirika na wakasema: Kwanini sisi tumefanya kazi nyingi kisha tukapata malipo machache? /ujira kidogo? Mwajiri akauliza: Jee nimekupunguzieni chochote katika haki yenu? Mayahudi na Manaswara Wakajibu: Hapana (Umetulipa kamili), Akasema Mwajiri: hizo ni fadhila zangu ninampa nimtakaye).

*Na katika sahihi vilevile kutoka kwa Abuu Hurairah (r.a) Amesema: Amesema Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w): (Allah Aliwapoteza waliokuwa kabla yetu kwa siku ya Ijumaa, siku ya jumamosi ikawa ni ya Mayahudi, na Jumapili ikawa ni ya Manaswara, Basi Allah akatuijia na akatuongoza kwa kutupa siku ya Ijumaa, na vilevile wao watatufuata sisi siku ya Qiyama, sisi ni wa Mwisho katika watu wa Duniani (tuliokuja baada yao) na tutakuwa wa Mwanzo (wao) siku ya kiyama).

*Na katika hadithi hii kuna nyongeza kutoka kwa Mtume (s.a.w) kwamba Alisema: (Imani inayopendeza zaidi mbele ya Allah ni Dini ya Uislamu iliyo nyepesi).

*Na kutoka kwa Ubayya Bin Kaabi(r.a) Amesema:(Shikamaneni na Njia/Uislamu na Mwenendo wa Mtume (s.a.w) kwani hakuna Mja yeyote aliyeshikamana na Uislamu na Mwenendo wa Mtume

(s.a.w) na akamtaja/akamkumbuka Allah mpaka macho yake yakabubujikwa machozi kwa kumuogopa Allah akaguswa na Moto. Na hakuna Mja yeyote aliyeshikamana na Uislamu na Mwenendo wa Mtume Rehma na Amani za Allh ziwe Juu Yake, ngozi yake ikasisimka kwa kumuogopa Allah isipokuwa atakuwa kama mfano wa Mti uliokauka majani yake, isipokuwa Madhambi yake yatadondoka kama yanavyo dondoka Majani katika Mti huu (uliotolewa mfano), na hakika kuwa na Msimamo/kati na kati katika jambo la kheri ni bora kuliko kufanya juhudi za kwenda kinyume na Uislamu na Mwenendo wa Mtume (s.a.w)).

*Na kutoka kwa Abuu dardai (r.a) Amesema: (Uzuri ulioje wa usingizi wa wenye akili na kufungua kwao! Ni vipi wanautia kasoro ukeshaji wa wapumbavu/wajinga na swaumu zao! Kiasi cha punje ndogo/dharrah ya wema pamoja na Ucha Mungu na yakini ni kubwa na bora na yenye nguvu/faida kuliko ibada za wenye kujidanganya kuwa wamefanya ibada hali yakuwa wamefanya kwa ujahili).

# MLANGO UNAOELEZEA UWAJIBU WA KUUFUATA UISLAMU

*Ni kauli yake Allah: (Na yeyote anaye tafuta Dini isiyokuwa Uislamu haitakubaliwa kwake. naye akhera atakuwa katika wenye kupata khasara).(Al- Imran: 85).

*Na kauli yake Allah Mtukufu: (Na kwa hakika hii ndiyo njia yangu Iliyo Nyooka.Basi ifuateni, wala msifuate njia nyingine zikakutengeni na Njia yake).(Al-An'aam: 153).

*Amesema Mujahid: Assubulu ni: Bida'a/Uzushi na Mambo yanayochanganya.

*Na kutoka kwa Mama wa Waumini Aisha (r.a) Amesema kwamba: Mtume wa Mwenyezi Mungu(s.a.w) Amesema: (Yeyote atakayezua jambo katika Dini yetu hii, Ambalo si katika Dini hii, basi litarudishwa (halitokubaliwa).Na katika tamko lingine Amesema Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w): (Yeyote atakayefanya Jambo Lolote ambalo si katika Jambo letu/la Uislamu basi Litarudishwa).Kapokea Bukhari na Muslim.

*Na amepokea Imamu Bukhari kutoka kwa Abuu Huraira (r.a) Amesema: Amesema Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w): (Umma wangu wote utaingia Peponi isipokuwa atakayekataa, ikaulizwa: Na ni nani atakayekataa?!!! Akasema Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w): (Atakayenitii Mimi ataingia Peponi, na atakayeniasi Mimi huyo ndiye atakayekuwa amekataa).

*Na katika hadithi iliyo sahihi kutoka kwa Ibni Abbasi(r.a) Amesema kwamba:Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w) Amesema: (Watu wanaochukiwa zaidi na

Allah ni watatu: (1) Mwenye kuegemea katika maasi ndani ya Haramu/sehemu tukufu.(2) Na Mwenye kutafuta katika Uislamu Mwenendo wa Ujahilia, (3) Na Mwenye kutafuta (kwa udi na uvumba ) damu ya Mtu Muislamu ili aimwage (amuue) bila ya haki (kuuwawa kwa dhulma). (Ameipokea hadithi hii Imam Bukhari).

*Na inaingia ndani yake kila ujahili wa moja kwa moja au wa muqayyad: Yaani kwa Mtu dhidi ya Mtu Mwingine, awe ni katika waliopewa kitabu au waabudiao Masanamu, au wasio kuwa wao kwa kila Mwenye kwenda kinyume na waliokuja nayo Mitume wa Allah.

*Na katika hadithi sahihi kutoka kwa Hudhaifa (r.a) Amesema: (Enyi kundi/kongamano la Wasomaji! Kuweni na Msimamo sasa; kwa hakika Mmeshatangulia utangulio wa mbali sana, ikiwa Mtachukua/Mtapita njia ya kulia na kushoto basi kwa hakika Mtakuwa Mmepotea upotevu wa Mbali sana).

*Na kutoka kwa Muhammad Ibni Wadhwaahi (r.a): Alikua akiingia Muskitini kisha anasimama kwenye halaqah/mduara wa elimu kisha anatoa ukumbusho na anasema: Ametupa habari Ibnu Uyainah kutoka kwa Mujaalid, kutoka kwa Ash-shaabiy, kutoka kwa Masruuq, amesema Abdullah – akikusudia Ibnu Masoud(r.a): Hakuna Mwaka wowote isipokuwa ule utakaokuja baada yake ni m'baya zaidi, usiseme mwaka mzuri/wa neema kuliko mwaka wowote, na usiseme Kiongozi Bora/Mzuri kuliko Kiongozi yeyote, lakini kuondoka kwa Wanachuoni wenu na Wabora wenu (ndiko kubaya) –kwasababu- Watu wanazusha na wanapima mambo kwa rai zao kisha wanauangamiza Uislamu na unakosa nguvu.

# MLANGO UNAOWEKA WAZI MAANA YA UISLAMU

*Ni kauli yake Allah: (Na ikiwa wakikuhoji basisema: Mimi nimeusalimisha/nimeuelekeza uso wangu kumwelekea Mwenyezi Mungu ungu na wanaonifuata). (Al-Imran: 20).

*Na katika hadithi sahihi kutoka kwa Ibni Omar(r.a) kwamba Mtume (s.a.w) Amesema: (Uislamu ni kushuhudia ya kwamba: Hapana Mola apasaye kuabudiwa kwa haki isipokuwa Allah, na kushuhudia ya kwamba Muhammad (s.a.w) ni Mtume wake, na usimamishe Swala (tano) na Utoe zakka na Ufunge mwezi wa Ramadhani na kuhiji nyumba tukufu ikiwa unaweza kupata njia ya kuifikia).

*Na katika sahihi kutoka kwa Abuu Huraira (r.a) kwamba: (Muisilamu ni Ambaye Waisilamu Wenzake Wamesalimika kutokana na Ulimi Wake na Mkono wake).

*Na kutoka kwa Bahzi Ibni Hakim, kutoka kwa Baba yake, kutoka kwa Babu yake, kwamba Alimuuliza Mtume (s.a.w)kunako/kuhusu Uislamu Akasema: (Ni kuusalimisha Moyo Wako kwa ajili ya Allah, na kuuelekeza uso Wako kwa Allah, na kusali Swala za Faradhi, na kutoa Zaka ya Faradhi). Imepokelewa na Imam Ahmad.

*Na kutoka kwa Abii Qilaba kutoka kwa Amri Ibn Abasa kutoka kwa Mtu wa Sham/Siria, kutoka kwa Baba yake kwamba yeye Alimuliza Mtume (s.a.w): (Ni nini Uislamu? Akajibu: Ni kuusalimisha moyo Wako kwa Allah, na wasalimike Waislamu kwa Ulimi Wako na mkono Wako), Akauliza tena: Ni Uislamu gani ulio bora? Akajibu Mtume (s.a.w) kuwa ni Imaani, Akauliza tena: Na ni nini hiyo Imani? Akajibu Mtume(s.a.w) kuwa: Ni kumuamini Allah na kuamini Malaika Wake, na kuamini Vitabu vyake, na kuamini Mitume Wake, na kuamini ufufuo baada ya mauti/kufa).

# MLANGO UNAOELEZEA KAULI YAKE ALLAH

*(Na yeyote anaye tafuta dini isiyo kuwa Uislamu haitakubaliwa kwake. Naye Akhera atakuwa katika wenye kupata khasara). (Al-Imran: 85).

*Kutoka kwa Abuu Huraira (r.a) amesema: Amesema Mtume (s.a.w): (Yatakuja matendo siku ya Qiyama, itakuja Swala itasema: Ee Allah! Mimi ndio Swala, Atasema Allah: hakika wewe upo katika kheri, kisha itakuja Swaumu, Atasema Allah: hakika wewe upo katika kheri, kisha yatakuja matendo mengine juu ya hayo, Atasema Allah: hakika wewe upo juu ya kheri, kisha utakuja Uislamu na Utasema: Ewe Mwenyezi Mungu: hakika Wewe ni Amani/Salam, na Mimi ndio Uislamu, hapo Atasema Allah: kwa ajili yako (Uislamu) Nachukua na Natoa (Naadhibu na Nalipa mema). Amesema Allah Mtukufu: (Na yeyote anaye tafuta dini isiyo kuwa Uislamu haitakubaliwa kwake. Naye Akhera atakuwa katika wenye kupata khasara). (Al-Imran: 85).Ameipokea hadithi hii Imam Ahmad.

*Na katika sahihi kutoka kwa Aisha (r.a) kwamba Mtume (s.a.w)Amesema: (Yeyote Atakayefanya jamdo lolote ambalo si katika Dini yetu litarudishwa/halitokubaliwa). Ameipokea hadithi hii Imam Ahmad.

## MLANGO UNAOELEZA UWAJIBU WA KUTOSHEKA KWA KUMFUATA MTUME -REHMA NA AMANI ZA ALLAH ZIWE JUU YAKE- KWA KILA KITU

*Na Kauli yake Allah Aliposema: (Na tumekuteremshia Kitabu hiki kinachobainisha kila kitu).(An-Nahl: 89).

*Na Amepokea Imamu An-Nasai na Wengineo kutoka kwa Mtume (s.a.w) ya kwamba: Alimuona Omar Ibn Khatwaab (r.a) akiwa na karatasi ya Taurati mkononi mwake, akamwambia: (Je Mna mashaka Ewe Ibnal-Khatwaab? Hakika nimekuijieni nayo ikiwa nyeupe safi, kama Mussa Angelikuwa Hai na mkamfuata, na mkaniacha mimi mngelipotea) na katika upokezimwengine: (Kama Mussa Angelikuwa Hai isingemuwezekania chochote isipokuwa kunifuata Mimi). Basi hapo Omar Akasema: Nimeridhia Allah kuwa ni Bwana, na Nimeridhia Uislamu kuwa ndio Dini, na Nimeridhia Muhammad kuwa ni Nabii.

# MLANGO UNAOELEZEA UBAYA WA KUTOKA KATIKA ULINGANO WA UISLAMU

Na kauli yake Allah: (Yeye (Mwenyezi Mungu) alikuiteni Waislamu tangu zamani, na katika hii (Qur'ani) pia).(Al-Hajj: 78).

*Kutoka kwa Al-Harith Al-Ash'ariy (r.a) kutoka kwa Mtume (s.a.w) Amesema: (Nakuamrisheni mambo matano Ambayo Allah Ameniamrisha kwayo (kuyatekeleza): (1) Kusikiliza (Mnachoambiwa).(2) Kutii (Mnachoamrishwa).(3) kupigana Jihadi katika njia ya Allah.(4) Kuhama/kufanya Hijra.(5) kushikamana/kuwa kitu kimoja, kwani Atakaye farakanisha/tenganisha Umoja kiasi cha shibri moja basi Atakuwa amevuakamba/ fundo la Uislamu katika shingo lake mpaka atakaporudi, na Atakayelingania ulinganio wa Kijaahiliya/(ukabila, makundi…) basi atakuwa ni Miongoni mwa kuniza Motoni, Mtu mmoja Akauliza: Ee Mtume wa Allah: hata kama Akisali na Akifunga? Akajibu: hata kama Akisali na Akifunga, Lingania ulingano wa Allah Ambaye Amekuiteni Nyinyi kuwa ni Waislamu, Waumini, Waja wa Allah). Ameipokea hadithi hii Imamu Ahmad na Tirmidhiyy na Akasema: Hadithi ni nzuri na ni sahihi.

*Na imekuja katika sahihi kwamba: (Yule Ambaye Atafarakiana na jamaa kiasi cha shibri moja basi kifo chake/atakachokufa ni kifo cha jaahiliyya -Ujinga-).

Na katika sahihi pia Amesema: (Je Mnalingania

Daawa ya ujinga na hali ya kuwa bado nipo nanyi?).

Amesema Abul-Abas: (Kila kinachotoka katika ulinganio wa Uislamu na Qur-ani kwa nasabu au mji jinsia/rangi, au madhehebu au njia basi hicho ni katika kujinasibisha na ujaahiliyya, bali walipo zozanawatu wa Makkah na Madina, Akasema Muhaajir: Enyi mnaostahiki kuwa Wahaajiriina! Na aksema Answariy: Enyi mnaostahiki kuwa Maanswari! Akasema Mtume (s.a.w): (Mnalingania ulinganio wa kijinga hali ya kuwa bado nipo nanyi!?) Na kwa jambo hilo Alikasirika sana Mtume (s.a.w).

## MLANGO UNAOELEZEA UWAJIBU WA KUINGIA KATIKA UISLAMU KIKAMILIFU NA KUACHA KILA KISICHO KUWA CHA UISLAMU

Na Amesema Allah Mtukufu: (Enyi mlio amini! Ingieni katika Uislamu kwa ukamilifu). (Al-Baqara: 208).

Na Amesema Allah Mtukufu: (Je! Huwaoni wale wanaodai kuwa wameamini yale yaliyoteremshwa kwako na yaliyoteremshwa kabla yako?). (An-Nisaa: 60).

Na Amesema Allah Mtukufu: (Siku ambayo nyuso zitakuwa nyeupe na nyuso -nyingine- zitakuwa nyeusi). (Al-Imran: 106). Amesema Ibnu Abbas (r.a): Watakao kuwa na nyuso nyeupe ni Ahlussunah na walioshikamana, na watakao kuwa na nyuso nyeusi ni watu wa bida'a/uzushi na kutofautiana).

*Kutoka kwa Abdullahi Ibn Omar (r.a) Amesema: (Yatawafikia Umma wangu yale yaliyowafikia banii Israail hatua kwa hatua, mpaka itafikia wakati ikiwa mmoja wao (katika Banuu Israail) alimwingilia mama yake wazi wazi, na kwenye Umma wangu atapatikana atakayefanya hivyo (atawaiga), Na hakika Banii Israail walifarakiana makundi sabini na mbili, na utatofautiana umma wangu makundi sabini na tatu, yote yatakuwa ni makundi ya motoni isipokuwa kundi moja tu, Maswahaba wakauliza: Ni kundi lipi hilo Ewe Mtume wa Allah? Akajibu: Ni lile ambalo lipo pamoja nami na Maswahaba zangu. -

litalo fuata mwenendo wake na maswahaba zake-).

Mawaidha mazuri yaliyoje! Lau kama mioyo ingeafikiana na maisha.Ameipokea Imamu Tirmidhiy,

na Ameipokea vilevile kutoka katika hadithi ya Muawiya kwa Ahmad na Abuu Daaud, na ndani ya hadithi hiyo: (Hakika atatoka mtu katika umma wanguatajibizana /munaadhara nao katika hizo dini zao kama anavyojibizana mbwa na mwenyewe/mwenye mbwa, kisha hapatobaki mishipa wala maungio isipokuwa vitaingia) na imeshatangulia hadithi: (Na mwenye kutaka katika Uislamu mwenendo wa ujaahiliya).

## MLANGO ULIOKUJA KUELEZEA KWAMBA BIDA/UZUSHI NI MBAYA/HATARI ZAIDI KULIKO MADHAMBI MAKUBWA

Na kauli yake Allah Aliposema: (Hakika Mwenyezi Mungu hasamehi(dhambi ya) kushirikishwa,na husamehe mengineyo kwa amtakaye). (An-Nisaa: 48).

Na kauli ya Allah Aliposema: (Ili wabebe mizigo yao kwa ukamilifu Siku ya Kiyama, na sehemu ya mizigo ya wale wanao wapoteza bila ya kujua. Angalia, ni maovu mno hayo wanayo yabeba!). (An-Nahl: 25).

*Na imekuja katika sahihi ya kwamba Mtume (s.a.w) Amesema kuhusu Makhawaarij: (Popote mtakapokutana nao wauweni).

*Na katika sahihi pia Mtume (r.a): (Amekataza kuwaua Viongozi wajeuri muda wa kuwa wanasimamisha Swala).

*Kutoka kwa Jariir, kutoka kwa Abdillahi kwamba Mtu Mmoja alitoa sadaka, kisha watu wakamfuata, basi Mtume (s.a.w) Akasema: (Atakaye anzisha katika Uislamu Sunna/Jambo zuri basi Atapata ujira wake na ujira wa yule aliyefanya baada yake/aliyemfata bila ya kupungukiwa na chochote katika ujira wao, na Atakaye anzisha katika Uislamu Sunna/Jambo baya, basi madhambi yatakuwa ni juu yake na atapata dhambi za Yule aliyemfuata baada yake bila ya kupungukiwa na chochote katika malipo/dhambi zao) Ameipoke hadithi hii

Imamu Muslim.

*Na katika mapokezi mengine ya Imamu Muslim kutoka kwa Abuu Huraira (r.a),na tamko la hadithi lipo hivi: (Atakayelingania katika Uongofu….. kisha Akasema;- Atakayelingania katika Upotevu).

## MLANGO UNAOELEZEA KUWA ALLAH AMETIA UGUMU WA TAUBA KWA MTU WA BID'A

Kuhusu swala hili limepokelewa kutoka katika hadithi ya Anas.Na akaeleza Ibnu Wadh-dhwaah kutoka kwa Ayub Amesema: (Tulikuwa na Mtu mmoja alikuwa anaiona rai Fulani kuwa ni nzuri kisha akaiacha, basi nikamuendea Muhammad Ibn Siirin nikamwambia: Je unahisi kwamba Fulani kaiacha rai yake? Akasema: hebu angalia ameenda kwenye rai gani (baada ya kuiacha rai ya mwanzo)? Kwasababu mwisho wa mazungumzo huwa ni makali zaidi ya mwanzo wake, (wanatoka katika uislmu kisha hawaurudii) Akaulizwa Ahmad Ibn Han'bal kuhusu maana hiyo Akasema: maana yake: Hawa wafikishwi katika kufanya tauba.

# MLANGO UNAOELEZEA KAULI YAKE ALLAH

(Enyi Mliopewa kitabu! kwanini mnabishana kuhusu Ibrahimu)?

Amesema Allah: (Enyi Watu wa Kitabu! Mbona mnabishana juu ya Ibrahim,na hali Taurati na Injili hazikuteremshwa ila baada yake? Basi hamzingatii?* Angalieni! Nyinyi mlibishana katika yale mliyo yajua. Mbona sasa mnabishana katika yale msiyo yajua? Na Mwenyezi Mungu ndiye ajuaye, na nyinyi hamjui kitu.* Ibrahim hakuwa Myahudi wala Mkristo, lakini alikuwa mwongofu Muislamu, wala hakuwa miongoni mwa washirikina).(Al-Imran: 65-67).

Na Amesema Allah: (Na nani atajitenga na mila ya Ibrahim isipokuwa anayeitia nafsi yake katika upumbavu, na kwa yakiniSisi tulimteuwa yeye katika dunia, na hakika yeye katika Akhera atakuwa miongoni mwa watu wema). (Al-Baqara: 130).

Na ndani ya mlango huu kuna hadithi ya khawaarij imekwisha elezwa, na ndani yake ni kwamba Amesema Mtume (s.a.w): (Watu/Jamaa wa baba Fulani si vipenzi vyangu, hakika vipenzi vyangu ni Wamchao Allah/WachaMungu).

Na vilevilekutoka kwa Anasi (r.a) kwamba Mtume (s.a.w) aliambiwa kuwa baadhi ya Maswahaba Wanasema: (Ama mimi siwezi kula nyama, na Mwengine Akasema: Nitasimama usiku kucha bila

kulala, na Mwengine Akasema: Ama Mimi siwezi kuoa wanawake, na Mwingine Akasema: Ama Mimi nitafunga bila kufungua, Akasema Mtume (s.a.w): (Lakini Mimi Nitasimama Usiku/Nitasali na Nitalala, na Nitafunga na Nitafungua, na Nitaoa wanawake, na Nitakula nyama, sasa basi atakaye acha mwenendo wangu si katika Sisi).

Basi hebu zingatia kwa makini, pale walipotaka baadhi ya Maswahaba kupuuzia na kuacha kabisa kuoa (ZUHDI) kwa ajili ya kushikamana na ibada, ikasemwa ndani yake maneno haya magumu kiasi hiki, na kitendo chake kikaitwa kuchukia Sunna, basi unadhani vipi itakuwa katika mambo mengine ya kuzushwa yasiyokuwa haya, na ni vipi itakuwa hali kwa wasiokuwa Maswahaba? (Ikiwa Maswahaba wamekemewa kiasi hiki, itakuwaje kwa wasiokuwa Maswahaba).

# MLANGO UNAOELEZEA KAULI YAKE ALLAH

(Basi elekeza uso wako katika Dini iliyo sawasawa).

Amesema Allah Mtukufu: (Basi uelekeza uso wako katika dini iliyo sawasawa, ndilo umbile Mwenyezi Mungu alilowaumbia watu; Hakuna mabadiliko katika maumbile ya viumbe vya Mwenyezi Mungu.Hii ndio dini ya haki lakini watu wengi hawajui). (Ar-Rum: 30).

Amesema Allah Mtukufu: (Na Ibrahim akawausia wanawe, na pia Yaaqub: Enyi wanangu! Hakika Mwenyezi Mungu amekuchagulieni Dini hii, basi msife ila nanyi mmekuwa Waislamu, wanyenyekevu). (Al-Baqara: 132).

Amesema Allah Mtukufu: (Kisha tukakufunulia ya kwamba ufuate mila ya Ibrahim,mwongofu, wala hakuwa miongoni mwa washirikina). (An-Nahl: 123).

Na kutoka kwa Ibnu Mas'oud(r.a) , kwamba Mtume (s.a.w) Amesema: (Hakika kila Nabii ana vipenzi katika Manabii, na Mimi kipenzi change katika hao Manabii ni Baba yangu Ibrahim na ni kipenzi cha Allah) kisha Akasoma kauli ya Allah: (Watu wanaomkaribia zaidi Ibrahim ni wale walio mfuata yeye na Nabii huyu na walioamini. na Mwenyezi Mungu ndiye Mlinzi wa Waumini).(Al-Imran: 68). Ameipokea Imamu Attirmidhiyy.

*Na kutoka kwa Abu Huraira(r.a) kwamba Mtume

(s.a.w) Amesema kwamba: (Hakika Mwenyezi Mungu haangalii viwiliwili vyenu, wala mali zenu, bali anaangalia nyoyo zenu na matendo yenu).Ameipoke hadithi hii Imamu Muslim.

*Na kapokea Bukhari na Muslim kutoka kwa Ibnu Mas'oud (r.a), Amesema: Amesema Mtume (s.a.w) kwamba: (Mimi nitakutangulieni/nitakuwa wa mwanzo kwenye haudhi/kisima/ cha maji, na watanyanyuka watu katika umma wangu kunisogelea, mpaka nitakapoinama ili niwape maji watazuiwa/wataondolewa dhidi yangu, kisha nitasema: Ee Mola Wangu! Ni watu wangu hawa, basi itasemwa: Hakika wewe hujuwi walichozusha baada yako).

*Na kutoka kwa Abuu Huraira(r.a)kwamba Mtume (s.a.w) Amesema kwamba: (Natamani lau ningewaona ndugu zangu, Maswahaba wakasema: Je sisi sio ndugu zako Ewe Mtume wa Allah? Akajibu: Nyinyi ni Maswahaba zangu, lakini ndugu zanguni wale ambao bado hawajaja) Wakauliza Maswahaba(r.a): Ni vipi utawajuwa ambao hawajaja kuwa ni katika umma wako? Akajibu Mtume (s.a.w): Mnaonaje kama mtu mwenye farasi wake anang'aa/ana uweupe katika paji lake la uso, na kati ya mgongo wake kuna uweusi kamili katika rangi yake (usio na doa), je hatomjua farasi wake? Wakajibu Maswahaba: ndio atamjua, Akasema Mtume (s.a.w): basi hakika wao watakuja siku ya kiyama wakiwa na nuru/wang'ara nyuso zao kutokana na athari ya udhu!!!! Na mimi nitawatangulia/nitakuwa wa mwanzo wao kuifikia Haudhi watafukuzwa watu siku ya kiyama kama

anavyofukuzwa ngamia mpotevu, nitawaita kuwaambia: njooni, basi itasemwa: Hakika wao walibadilisha (muongozo/mwenendo) baada yako, Nitasema: (wawe) mbali na mimi).

*Na katika mapokezi ya Imamu Bukhariy: Nilipokuwa nimesimama mara likatokea kundi mbele yangu, (nikawashangaa) mpaka pale nilipowajua akatokeza Malaika kati yangu na yao Akasema: Njooni (nifateni) Nikasema (Mtume): akamuuliza: unakwenda nao wapi? Akajibu Malaika: Motoni kwa jina la Mungu, Nikasema (Mtume): Ni nini jambo lao/wamefanya nini? Akajibu Malaika: hakika wao walirejea nyuma (waliacha mafundisho yako) baada yako, kisha likatokea kundi linguine -akaelezea mfano wa maelezo ya hapo juu- Akasema: basi sikuwa na muona yeyote anasalimika isipokuwa ni mfano wa ngamia asiye na mchungaji).

*Na katika hadithi ya Ibni Abbas(r.a) Nitasema kama alivyosema Mja Mwema wa Allah: (Na mimi nilikuwa shahidi juu yao nilipo kuwa nao. Na uliponifisha ukawa Wewe ndiye Muangalizi juu yao. Na Wewe ni shahidi juu ya kila kitu).(Al-Maaida: 117).

*Na hadithi Maarufu Amesema Mtume (s.a.w): (Hakuna mzaliwa yeyote anayezaliwa isipokuwa huzaliwa katika umbile la Uislamu, isipokuwa wazazi wake ndio ambao humfanya mtoto kuwa ni Myahudi au Mnaswara au Mmajusi kama anavyozaa Mnyama; mnyama mwenye viungo kamili bila ya mapungufu

yoyote, hamtamhisi (katika uzao) mapungufu yoyote mpaka muwe nyinyi ndio wenye kuwapa/kuwasababishia mapungufu) Kisha akasoma Abuu Hurairah(r.a) (Ndilo umbile Mwenyezi Mungu alilowaumbia watu; (yaani dini hii ya kiislamu)..). (Ar-Rum: 30).Hadthi imepokelewa na Imamu Bukhariyy na Muslimu.

*Na kutoka kwa Hudhaifa, Allah amuwie radhi Amesema: (Watu walikuwa wakimuuliza Mtume (s.a.w) kuhusu Kheri, na mimi nilikuwa nikimuuliza kuhusu Shari, kwa kuhofia isije nifika hiyo shari, nikasema: Ee Mjumbe Wa Allah! Hakika sisi tulikuwa katika ujahilia na shari/ubaya, lakini Allah akatuletea kheri hii (tukaoongoka) Basi je baada ya Kheri hii itakuja Shari? Akajibu: Ndio, nikasema tena: na baada ya Shari hiyo kuna Kheri? Akajibu: Ndio, na ndani yake kunadakhnu ukungu/uharibifu! Nikamuuliza: na nini hiyo dakhnu yake? Akajibu: watakuwepo watu watakaokuwa na Mwenendo usio kuwa Mwenendo Wangu, na watafata Uongofu usiokuwa Uongofu Wangu, utawajua katika wao na utawachukia, nikauliza: basi je baada ya Kheri hiyo kuna Shari? Akajbu; Ndio, ni fitna ya vipofu/majaahili na walinganiaji katika Milango ya Moto wa Jahannam, Yeyote atakayewakubalia ulingano wao watamptupia katika Jahannam, Nikasema: hebu tuwekee wazi/tupe sifa zao Ewe Mjumbe wa Allah, Akasema: Ni watu katika sisi, na wanazungumza kwa lugha yetu, nikasema: Ewe Mjumbe wa Allah ni nini unaniamrisha ikiwa nitaifikia hali hiyo? Akasema: Shikamana na

umoja wa Waislamu na Kiongozi wao, Nikauliza: na ikiwa (wakati huo) hakuna Umoja wala Kiongozi? Akajibu:Jiepushe na makundi yote hayo (yaliyopo) na hata kama utaung'ang'ania mzizi wa mti kwa meno mpaka yakufike Mauti na wewe upo katika hali hiyo).(Imepokelewa na Bukhariy na Muslimu).

Na amezidisha Imamu Muslim katika upokezi mwengine: Kisha nini kitafuata? Akijibu: atatokea Dajjali akiwa na Mto wa Maji na Moto, basi atakaye angukia katika moto wake atakuwa amestahikiujira,(amefaulu) Nikauliza kisha ni nini (kitafuata)? Akajibu kuwa: hicho sasa ni kiyama).

Akasema Abuu A'aaliyah:(Jifundisheni Uislamu, na mtakapojifundisha basi msiuchukie, na shikamaneni na njia iliyonyooka kwani huo ndio Uislamu ulio sawasawa, na wala msiyumbe yumbe/msitikisike kulia na kushoto, na shikamaneni na Sunna/Mwenendo wa Nabii Wenu, na jiepusheni na haya matamanio) Mwisho wa maneno yake.

Zingatia maneno haya ya Abuu A'aaliyah kwa uzito wake, na juwa muda wake ambao alikuwa anatahadharisha kuhusu matamanio, ambayo atakayeyafata basi atakuwa ameuchukia Uislamu, na hutafsiriwa Uislamu kwa Sunna, na khofu yake katika kutoka kwenye Kitabu na Sunna juu ya mataabi'ina wakubwa na wanachuoni wao, inakubainikia sasa kuali yake Allah: (Kumbukeni pale Mola wake Alipomwambia nyenyekea) (Al-Baqara: 131).

Na kauli yake Allah:(Na Ibrahimu akawausia haya

wanawe, na Yaaquubu (pia aliwausia wanawe) Enyi wanangu! Hakika Allah amekuchagulieni Dini hii, basi msife ila ni waislamu/wanyenyekevu). (Al-Baqara: 132).

Na kauli yake Allah: (Na ni nani atajitenga na Mila ya Ibrahimu (akaichukia Dini hii ya Kiislamu) isipokuwa anayeitia nafsi yake katika upumbavu)? (Al-Baqara: 130).

Na mifano ya misingi hii mikubwa ndio asili/msingi wa Misingi na watu wameghafilika nayo, na kwa kuijua kwake imebainika maana ya hadithi nyingi katika mlango huu na mfano wake, ama mwanadamu ambaye anayeisoma na mfano wake na hali ya kuwa ni mwenye kutulia/kuamini kuwa haimpati na anaidhania misingi hiyo kwa watu waliokuwepo tangu zamani kisha wakaaminisha kuadhibiwa na Allah, basi nahawaaminishi adhabu ya Allah isipokuwa watakuwa ni watu wenye khasara.

*Na kutoka kwa Ibni Mas'oud(r.a) amesema: Mtume (s.a.w) Alituchorea mustari kisha Akasema: Hii ndio njia ya Allah, kisha akachora tena mistari mingine upande wa kulia na kushoto kisha akasema: hizi njia (mnazoziona), kwenye kila njia kuna Shetani anawalingania watu waiendee njia hiyo, kisha akasoma: (Na hakika hii ndio njia yangu iliyonyooka, basi ifuateni, na wala msifuate vinjia vingine vikakutoeni katika njia ya Allah). (Al-An'aam: 153).Ameipokea hadithi hii Imamu Ahmad na Annasaai.

## MLANGO UNAOELEZEA UGENI WA UISLAMU NA UBORA WA WATAKAO ONEKANA NI WAGENI KATIKA UISLAMU

Na Amesema Allah: (Basi mbona hawakuwamo katika watu mbele kabla yenu, watu wenye akili, wenye kukataza uharibifu katika nchi? Isipokuwa wachache tu miongoni mwao ambao ndio tuliowaokoa..).(Hud: 116).

Na kutoka kwa Abuu Hurairah(r.a) kutoka kwa Nabii Muhammad (s.a.w): (Uislamu ulianza Mgeni na utarudi kuwa Mgeni kama ulivyoanza, basi ni ubora ulioje kwa watakao onekana ni wageni wa Uislamu)Ameipokea Imamu Muslimu

Na amepokea Imamu Ahmad katika hadithi ya Ibni Mas'oud(r.a): (Ni nani hao watakaoonekana ni wageni katika Uislamu? Akajibu: Ni wenye kujiepusha na ukabila na wenye kutengeneka pale watu wanapoharibika).

Na katika hadithi alio ipokea Imamu Tirmidhiy kutoka kwa Kathiirbin Abdullah kutoka kwa baba yake kutoka kwa babu yake: (Basi ni ubora/uzuri ulioje wa watakao shikamana na Uislamu, ambao wanatengeneza yale waliyoyaharibu watu wengine katika sunna zangu).

Na kutoka kwa Abii Umaya(r.a) amesema: (Nilimuuliza Abaa Tha'alaba: Unasemaje kuhusu aya hii: (Enyi mlioamini! Lililo lazima juu yenu ni nafsi

zenu, hawakudhuruni waliopotoka/waliopotea ikiwa nyinyi mmeongoka...). (Al-Maaida: 105). Akasema: Wallahi kwa hakika Umemuuliza Mwenye kulijua jambo hilo: kwani Nilimuuliza Mtume(s.a.w) Akasema: Bali amrishaneni mema na mkatazane mabaya mpaka mtakapomuona mchoyo Mwenye kuutii uchoyo wake na Mwenye kutii hawaa zake/matamanio yake na Mwenye kuipenda Dunia na Mwenye kujiona kwa rai kila Mwenye rai yake, basi ni juu yako nafsi yako kuikinga na maasi, na uachane na mambo ya watu, kwani hakika mbele yenu kuna Masiku yanakuja, Mwenye kuwa na subira katika Masiku hayo ni mfano wa mtu aliyeshika kaa la Moto, Mwenye kuyafanyia kazi (Hayo aliyoshikamana nayo katika dini) atapata ujira wa watu hamsini ambao wanatenda mfano wa matendo yenu, tukauliza: ni katika sisi au katka wao? Akajibu : ni katika Nyinyi). Ameipokea hadithi hii Abu Daud na Tirmidhy.

Na amepokea IbnWadhwaah kwa maana yake (hadithi) katika hadithi ya IbnOmar(r.a) na tamko lake (hiyo hadithi): (Hakika baada yenu Nyinyi kuna masiku yanakuja, Mwenye kuwa na Subira katika masiku hayo, Mwenye kushikamana na dini yake ni mfano wa yale mliyonayo/yanayokusibuni hii leo, atapata ujira wa watu hamsini katika nyinyi, kisha akasema:Ametupa habari Muhammad Ibn Saiid, Ametupa habari Asad, amesema Sufian Ibnu Uyainah, kutoka kwa Baswariy kutoka kwa Saiid ndugu yake Hasan.. Amesema: Hakika nyinyi leo hii mpo juu ya hoja kutoka kwa Mola wenu, Mnaamrisha mema na

mnakataza mabaya na mnapigana Jihadi katika njia ya Allah, na haijakudhihirikieni vilevi viwili: (1) kilevi cha ujinga na (2) kilevi cha kupenda maisha ya dunia, na mtageuzwa kutoka katika hali hii mliyonayo/mtabadilishwa, basi Mwenye kushikamana na Kitabu/Quraan na Sunnah siku hizo zijazo atapata ujira wa watu hamsini, ikaulizwa: Miongoni mwao? Akasema: la Bali ni katika Nyinyi).

Na ana mtiririko mwingine kutoka kwa Amuaafiriyy amesema: Amesema Mtume (s.a.w): (Uzuri ulioje kwa watakaoonekana ni wageni katika Uislamu, ambao wanashikamana na Kitabu/Quraan inapoachwa na wanazifanyia kazi Sunna pindi zinapozimwa/zinapoachwa).

# MLANGO UNAOTAHADHARISHA BID'AA/UZUSHI

Kutoka kwa Irbaadh Ibni Saariyya (r.a) Amesema: Mtume (s.a.w) Alitupa Mawaidha mazito sana, tukasema: Ewe Mjumbe wa Allah! Kana kwamba ni Mawaidha ya Mwenye kuaga! Basi tuusie, Akasema: (Ninakuusieni kumcha Allah Mtukufu, na kuwa wasikivu na wenye kutii, na hata kama Mtawekewa Mtumwa ndio awe kiongozi wenu, na hakika atakayeishi maisha marefu miongoni mwenu basi ataona tofauti/ikhtilafu nyingi sana, basi ni juu yenu kushikamana na Sunna zangu na Sunna za Makhalifa Waongofu, zishikeni kwa Magego, na Tahadharini/jiepusheni na kuzua mambo (katika dini), kwani hakika kila uzushi ni upotovu).Amesema Attirmidhiyy: hadithi ni nzuri sahihi).(

Na kutoka kwa Hudhaifa Amesema: (Kila ibada ambayo hawaifanyi Maswahaba wa Muhammad basi msiifanye kuwa ni ibada, kwani wa Mwanzo hakumuachia wa Mwisho chochote, basi mcheni Allah enyi kundi la wasomaji, na chukueni njia ya wale waliokuwa kabla yenu (watu wema) (Ameipokea Abuu Daaud).

Na Amesema Addaarimiyy: Alitupa habari Alhakam Ibn Mubarak, Ametupa habari Amru Ibn Yahyaa, Amesema: (Nilimsikia baba yangu akimzungumzia baba yake Akasema: Tulikuwa tukikaa kwenye mlango wa Ibni Mas'oud kabla ya swala ya Asubuhi, basi akitoka tunaenda naye mpaka msikitini,

mara akatuijia Abuu Muusaa Al'ash'ariy akauliza: Je Baba Abdilrrahman ameshatoka? Tukamjibu: bado hajatoka, basi akakaa pamoja nasi, alipotoka Akasema (Abu Musaa Al-Ash'ariy): Ewe Baba Abdilrrahman: Mimi nimeona jambo msikitini nimelichukia/ limenichukiza, na namshukuru Allah sikuona isipokuwa ni kheri/zuri, akamuuliza: ni jambo gani hilo? Akajibu Abuu Muusaa Al'ash'ariy: ukiendelea kuishi utaliona, kisha akasema: Nimewaona watu Msikitini wamekaa Duara wanasubiri swala, katika kila halaqah/duara kuna mtu na mikononi mwao wana vijiwe vidogo vidogo huku Akisema: Semeni Allahu Akbaru mara 100)(wanasema Allahu Akbaru mara 100) kisha Anasema: Semeni Laa ilaaha illa Allahu mara 100, nao wanasema: Laailaaha illa Allahu mara 100, kisha Anasema: Semeni Subhaana Allah mara 100, nao wanasema: Subhaanallahu mara 100, basi Baba Abdirrahman akamuuliza Abuu Muusaa Al'ash'ariy: uliwaambia nini (baada ya kuwaona wanafanya hivyo)? akajibu: sikuwaambia kitu, nilikuwa nasubiri Amri yako, Abu Abdirrahman akamwambia AbuMusaa Al-ash'ariy: kwanini usiwaamrishe wakahesabu makosa/madhambi yao na ukawadhaminia kwamba hakitapotea chochote katika mema yao? Kisha akaenda mpaka akafika kwenye hiyo halaqah/vikundi akawaambia: Ni nini hiki (mfanyacho)? Wakamjibu: ni vijiwe tunahesabia Takbir na Tahliil na Tasbiih, Akawaambia: basi hesabuni makosa yenu na mimi nakudhaminieni/nakuhakikishieni kuwa hakitapotea chochote katika mema yenu, Ole wenu Enyi Ummat Muhammad! Ni maangamivu ya haraka kiasi gani!

/mmeangamia haraka sana, hawa maswahaba wa Nabii wenu Rehma na Amani za Allah ziwe Juu Yake bado wapo wa kutosha, na hizi ni nguo zake hata hazijachakaa/hazijaisha, na vyombo vyake havijavunjwa, naapa kwa yule Ambaye nafsi yangu ipo mikononi Mwake: hakika nyinyi mpo katika Mila/Dini ambayo ni ongofu zaidi kuliko mila/dini ya Muhammad au mmefungua mlango wa upotevu, wakasema wale watu: tuna apa kwa jina la Allah Ewe Baba Abdilrrahman hatukukusudia isipokuwa ni kutafuta kheri tu, akawaambia: ni wangapi walikuwa ni wenye kutafuta kheri na hawakuipata? Hakika Mtume Rehma na Amani za Allah ziwe Juu Yake Alituhadithia/alituambiakwamba kutakuwa na watu ambao watakuwa wanasoma Qur-ani lakini haivuki kwenye koromeo zao, Akala kiapo akisema: huenda wengi wao ni miongoni mwenu.

Amesema Amru Ibn Salama: Tuliwaona wengi katika watu hao wakitushutumu/wakitudharau siku ya nahrawaani(Nahrawani ni vita aliyopigana Ally Ibn Abii Twalib na makhawaarij) wakiwa pamoja na makhawaarij.

Hapa ndio mwisho wa kile kilichowezekana.

Rehma na Amani za Allah zimuendee Nabii Muhammad pamoja na familia yake na maswahaba zake na Waislamu wote watakaofuata mwenendo wake hadi siku ya kiyama, Tuna muomba Mwenyezi Mungu atujaalie tuwe katika hao Amiin.